

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI  
(VETA)



MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 20 mwezi 02 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha VETA DSM, S.L.P. 40274,  
DAR-ES-SALAAM ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya  
Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana  
kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

ALLY SAIDI BEWA S.L.P. \_\_\_\_\_, DAR-ES-SALAAM  
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundu") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya  
PANGANI;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za  
nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya PANGANI;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundu kwa ajili ya kazi ya  
KUTENGENEZA NA KUFUNGA MAGRILI YA MILANGO NA  
MADIRISHA NYUMBA YA WAAZIMU (SEMI DETACHED HOUSE)

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundu nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo  
wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinavyoonyesha namna kazi  
itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 915,000, Fundi atafanya kazi ya UFUNDA kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu. Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundi;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi;na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio":5% ya Gharama ya Ufundi.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

(a) Fundi atakabidhiwa eneo la kazi tarehe 19 mwezi 02 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.

(b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 30 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.

(c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao:

wowote utatoa Notisi ya siku kumi na nne ya kupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi (arbitration).

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA

DSM

Jina: Kalim Guma Saini: [Signature]

Wadhifa: Sho Tarehe: 20/02/2022

REGIONAL VOCATIONAL TRAINING & SERVICES CENTRE DAR-ES-SALAAM

Mbele ya (Shahidi)

Jina: Fanda R. Allate Saini: [Signature]

Wadhifa: Mhandisi wa Madi Tarehe: 20/02/2022

IMESAINIWA NA FUNDI

Mbele ya

Jina: ALLY SAIDI BFWA Saini: [Signature]

Wadhifa: FUNDI Tarehe: 20/02/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: Goodluck Cyprian Mushi Saini: G. C. Mushi

Wadhifa: FUNDI Tarehe: 20/02/2022